



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII  
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA



NOVEMBER 14, 2018

**TANGAZO**

**UUZAJI WA MITI AINA YA MIKARATUSI (EUCALYPTUS SPECIES) KWA NJIA YA MNADA KATIKA ENEO LA UTAFITI WA MITI (KWAMARUKANGA) KOROGWE TANGA.**

1. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inatarajia kuuza jumla ya miti **2,502** yenye jumla ya meta za ujazo **2257.41** aina ya Mikaratusi (Eucalyptus) yenye kipenyo kati ya sm 16 – 46 iliyopo katika eneo la Utafiti wa Miti ya Mikaratusi – Maili Kumi, - Korogwe. Mauzo haya yatafanyika tarehe 29 Novemba 2018 katika Kituo cha Utafiti wa Mikaratusi – Maili Kumi, Kwamarukanga Korogwe saa tano (5:00) asubuhi. Uuzaji utafanyika kwa njia ya mnada kwa kuzingatia Kanuni 31 (ii) ya kanuni za sheria ya misitu za mwaka 2004. Miti hii ya mikaratusi itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.
2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo haya kwa njia ya mnada anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi kwenye bahasha iliyofungwa na juu yake kuandikwa MNADA WA MITI, kuonyesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatanisha leseni ya biashara, usajili wa biashara ya mazao ya misitu (poles/timber) (2018/19) na cheti cha utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN).
3. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania inawaalika wenye nia ya kushiriki mnada kutuma maombi yao kwa anuani ifuatayo: **Mkurugenzi Mkuu, TAFORI, S. L. P. 1854, MOROGORO**. Mnunuzi atatakiwa kuonyesha katika maombi yake bei ya jumla ya kununua idadi ya miti kwa Kitalu anachohitaji kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo (Jedwali Na. 1):

### Jedwali Na. 1: ORODHA YA VITALU, IDADI YA MITI NA BEI ZA AWALI

Na.	Jina la Kitalu	Idadi ya Miti	Ujazo (CBM)	Bei ya Awali/ Kitalu
1	Kitalu A	226	193.37	8,397,453
2	Kitalu B	239	212.24	9,620,456
3	Kitalu C	179	143.87	6,089,350
4	Kitalu D	185	126.47	4,979,034
5	Kitalu E	151	112.02	4,646,909
6	Kitalu F	397	407.76	19,127,179
7	Kitalu G	379	355.91	16,506,307
8	Kitalu H	144	144.77	6,886,285
9	Kitalu I	602	561.01	25,440,793
	<b>JUMLA</b>	<b>2502</b>	<b>2257.41</b>	<b>101,693,766</b>

- Izingatiwe kwamba, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine waliowasilisha maombi au yeye mwenyewe kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.
- Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika Kituo cha Utafiti wa Misitu, Kituo kidogo cha Kwamarukanga siku ya Alhamisi tarehe 29 Novemba 2018. Mnada utaendeshwa kwa kufuata sheria ya misitu sura ya 323.
- Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya Mkaratusi katika mnada huu hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50(1) ya mwaka 2004. Kusafirisha Mazao nje ya nchi ni baada ya kuyachakata kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na 69 la Mwaka 2006.

7. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya Mkaratusi katika mnada huu atawajibika kuchukua hati ya malipo (Bill) pamoja na masharti ya uvunaji toka Ofisi ya TAFORI iliyoko eneo la mnada.
8. Makampuni na Watu binafsi wanakaribishwa kutembelea eneo la miti inayouzwa wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi mpaka saa tisa (9:00) alasiri. Msimamizi wa Kituo au Afisa aliyeteuliwa atakuwepo kwa ajili ya maelezo zaidi.
9. Bei ya miti ya Mkaratusi iliyoonyeshwa katika Jedwali Na 1 inajumuisha malipo yote yaani 'VAT', CESS, FOREST ROYALTY na LMDA.
10. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya jumla kuu kwa kitalu husika na kuwasilisha nakala ya hati ya malipo (Bank Pay In Slip) ndani ya siku tatu, fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yote yatafanyika kwa kupitia akaunti ya Taasisi kama ifuatavyo:  
  
**Jina la Akaunti: TAFORI GENERAL ACCOUNT**  
**Namba ya Akaunti: 22101100006**  
**Bank: NMB**
11. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Taasisi [www.tafari.or.tz](http://www.tafari.or.tz)
12. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya mwezi mmoja baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia mia moja (100%).

13. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Alhamisi, tarehe 29 November 2018 saa tatu (3:00) asubuhi. Wanunuzi watakochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika majadiliano ya mauzo.

**Imetolewa na,**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu,

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI).

